

# Mwongozo wa Kuchanganua Habari za Upotoshaji.

Mwongozo wa hatua kwa hatua wa jinsi ya kutambua vipengele vikuu vya mashambulizi ya upotoshaji yanayolenga waandishi wa habari na vituo vya habari.

# Mwongozo wa Haraka

Hizi hapa hatua nne ambazo waandishi, watafiti, na wengine wanaochunguza kampeni za habari na taarifa potofu dhidi ya vyombo vya Habari wanaweza kuchukua:

## 1 Elewa muktadha

## 2 Chambua muda, jukwaa na mbinu zilizotumika kusambaza upotoshaji

## 3 Tambua wahusika waliohusika

## 4 Gundua aina za hoja/mambo yanayozungumziwa

Mwongozo huu ni wa hatua kwa hatua kwa waandishi wa habari na watafiti wanaochunguza kampeni za upotoshaji na uchafuzi wa jina dhidi ya vyombo vya habari. Unatoa mfumo wa kutambua mbinu, mbinu za kiufundi, na taratibu (TTPs) nyuma ya kampeni za upotoshaji. Kwa kufanya hivyo, unalenga kusaidia juhudi za kufichua na kupinga kampeni hizi ambazo zinatumiwa sana kuwalenga waandishi wa habari na kudhoofisha imani ya hadhira katika habari za ukweli.

Miongozo hii **haitatui matatizo ya kila aina** kwani upotoshaji unabadilika kila wakati na teknolojia mpya. Hii ni nakala inayoendelea kubadilishwa, itakayosasishwa kadri mbinu mpya zinavyoendelea.

# 1 Elewa muktadha

**Lengo hapa ni kuelewa ikiwa na kwa namna gani mashambulizi ya upotoshaji dhidi ya vyombo vya habari yanavyoakisi mikakati mipana zaidi ya kudhoofisha imani ya umma kwa vyombo vya habari. Hizi ni sehemu kuu ambazo kwa kawaida tunajaribu kuzitambua:**

## Matukio na kauli muhimu ndani ya kipindi cha mashambulizi

- Tambua matukio ya nyuma yanayochangia mazingira ambapo waandishi wa habari wanalengwa kwa kuripoti kwao. Haya yanaweza kuwa uchaguzi, harakati za maandamano au migogoro ya kijamii au changamoto (k.m. uhamiaji, masuala ya kijamii).
- Tambua mada maalum au mjadala wa umma unaoonekana kuanzisha shambulio.
- Tambua kauli za wanasiasa, watu mashuhuri au wahusika wengine wa kisiasa zinazounda mazingira yanayohalalisha mashambulizi dhidi ya waandishi wa habari.

## Muktadha mahsusi wa kisiasa na kijamii

- Tambua ajenda za wahusika wa kisiasa au wengine wanaohusiana na kampeni ya upotoshaji.

## Vyombo vya habari na njia za mitandao ya kijamii zinazotumia kusambaza hadithi za uongo

- Angalia majukwaa ya mtandaoni pamoja na vyombo vya habari vya kawaida na vile vya “mbadala”.

# 2 Chambua muda, jukwaa na mbinu zinazotumika kusambaza upotoshaji

**Watafiti na waandishi wa habari wanapaswa kutengeneza muda wa shambulio ili kuelewa vizuri mtiririko wa kampeni ya upotoshaji. Pia wanapaswa kutambua majukwaa yaliyotumika kupeleka kampeni na vichocheo vilivyotumika kueneza kampeni kama vile hashtagi, memes na video au sauti zilizotengenezwa kwa teknolojia ya AI.**

### Tengeneza muda wa shambulio: Tambua na eleza (ma)tukio muhimu linalohusiana na mashambulizi na tengeneza mtiririko wa muda wa jinsi tukio hilo lilivyotokea.

Kwanza kabisa, zungumza na mlengwa wa kampeni ili kupata maelezo ya awali ya shambulio. Waandishi wa habari waliolengwa mara nyingi wana uelewa mzuri wa vipengele muhimu vya kampeni za upotoshaji na wanaweza kutoa muktadha wa muhimu wa takuio zima, ikisaidia kutengeneza ratiba ya awali ya kampeni. Ikiwa mlengwa alikuwa ni shirika la habari, zungumza na wanachama wa wafanyakazi husika: wahariri, waandishi wa habari, wasimamizi wa jamii au wataalamu wa usalama wa kidijitali.

Angalia kazi ya mwandishi wa habari iliyotumika kuchochea kampeni ya uchafuzi wa jina dhidi ya mwandishi mwenyewe au kituo cha habari.

Angalia ni lini na wapi (majukwaa, tovuti nk.) matukio ya kwanza ya mashambulizi yalitambuliwa na uyaorodheshe kwa mpangilio wa muda. Kwa kufanya hivyo, eleza jinsi kampeni ilivyotekelezwa kwenye majukwaa mbalimbali katika kipindi ambacho shambulio lilidumu.

Baadhi ya vyombo vya habari huhifadhi rekodi za mashambulizi na unyanyasaji kwa muda mrefu, hivyo hakikisha kuzikagua na kujumuisha matukio yoyote yanayohusiana na shambulio linalochunguzwa.

### Tambua njia za mashambulizi na unyanyasaji

Tafuta kwenye mitandao ya kijamii kurasa na profaili zinazotaja mlengwa: Telegram, X, YouTube na Facebook ni kawaida (hadi mwaka 2024) lakini pia angalia Instagram, Threads, Reddit, TikTok, WhatsApp na majukwaa mengine kulingana na umaarufu wao katika eneo muhusika analoishi na kufanya kazi.

Mashambulizi na unyanyasaji mara nyingi hufanywa kupitia vyombo vya habari vya "mbadala" na tovuti zinazotumia majina ya vyombo vya habari vingine. Ikatokea taarifa kuhusiana na majukwaa haya hazieleweki, tumia taarifa zinazopatikana (orodha rasmi nk) kujaribu kubaini umiliki na msingi wa kihariri wa vyombo/chaneli hizo.

## Tambua vipengele vilivyotumika kueneza kampeni ya uchafuzi kwa haraka zaidi

Tafuta hashtagi, memes, picha zilizobadilishwa, video, matusi, taarifa binafsi za mtu, video au sauti zilizotengenezwa kwa teknolojia ya Akili Mnemba kwenye majukwaa tofauti. Kumbuka kwamba sio kila chapisho ni tishio dhahiri hivyo rekodi pia matukio ya vitisho visivyo dhahiri au mbinu nyingine za kutisha kama vile doxxing (sehemu ya taarifa za kibinafsi imewekwa wazi kwa kawaida barua pepe au namba ya simu ya mwandishi wa habari anayelengwa) ili kupata picha nzima ya kile kinachosemwa.

Angalia kama kuna kesi za SLAPP au vitisho vya mashtaka vinavyohusiana na mashambulizi.

Angalia kama mwandishi wa habari au kituo cha habari kimekuwa kikilengwa hivi karibuni na mashambulizi ya kimtandao.

Tambua taarifa za waandishi wa habari, kauli rasmi na taarifa za vyombo vya habari za wanasiasa au wahusika muhimu wa shambulio

MAZOEA BORA

## Hifadhi URL za matukio yote ya mashambulizi au taarifa za uongo zilizolengwa kwa mlengwa.

Unaweza kuunda mfumo wa ndani wa kuhifadhi au kutumia majukwaa kama vile [https://ghostarchive.org/](https://ghostarchive.org/) au [https://archive.org/](https://archive.org/)

# 3 Tambua Wahusika Waliohusika

**Kwa sababu ya uchunguzi ni muhimu kutambua wale waliochochea na/au kuanzisha shambulio na wale waliotekeleza. Wahusika hawa wanaweza kuwa vikundi vya kisiasa, wavuti, kurasa za mitandao ya kijamii zisizo na majina halisi, vyombo vya habari vya mbadala na wahusika wengine muhimu wanaohusishwa na kampeni ya upotoshaji.**

## Tambua na eleza wahusika wenye ushawishi zaidi waliochochea kampeni ya upotoshaji

- Andika wasifu mfupi, uhusiano wa kisiasa au mwingine, akaunti za mitandao ya kijamii na wafuasi wa mtandao huo, kauli muhimu kwa kila mhusika wa kisiasa aliyeainishwa.
- Tafuta matukio ambayo wahusika hawa waliomba wafuasi wao kulenga mwandishi wa habari au kituo cha habari.

## Tambua na eleza wahusika muhimu (wa mbadala) wa vyombo vya habari waliokuwa wakiripoti kwa upendeleo kuhusu shambulio na kuunga mkono hoja za upotoshaji zilizokuwa zikisambazwa

- Angalia maelezo ya mmiliki wa tovuti na uzingatiaji wake wa sheria za kitaifa.
- Angalia uwepo kwenye mitandao ya kijamii ikiwa ni pamoja na wafuasi wake.
- Angalia Internet Archive (Wayback Machine) kwa toleo za awali za tovuti. Hii inaweza kufichua kurasa za “kuhusu” zilizokuwa hai hapo awali lakini baadaye zikafutwa na wasimamizi.
- Angalia hifadhidata za vyombo vya habari kama vile Newsguard kwa ukujifunza zaidi.

MAZOEA BORA

## Fanya uchambuzi wa miundombinu ya wahusika wakuu pamoja na tovuti. Uchambuzi huu unaweza kuhitaji kushirikiana na wataalamu wa IT au wa OSINT na inaweza kujumuisha pamoja na mengine:

- Uchambuzi wa DNS wa tovuti za propaganda
- Utafutaji wa picha, nembo na michoro mingine kujua ambako zinawezakuwa zilitumika awali katika machapisho mengine
- Utafutaji wa Kikoa na IP


MAZOEA BORA

## Fanya uchambuzi wa mitandao ya kijamii ili kugundua uhusiano na wahusika na uhusiano wao

Zana na kampuni nyingi za kitaalamu zinaweza kufanya uchambuzi huu kulingana na mahitaji yako. Hizi zinawezakusaidia katika kutambua wahusika waliokosekana wakati wa utafutaji wa awali na zinaweza kuonyesha usambaaji wa jumbe unaohusiana na mashambulizi. Hapa kuna orodha ya programu ambazo tumefanya kazi nazo:

- Gephi - The Open Graph Viz Platform
- NodeXL
- Gerulata
- Kivu.tech

**Mfano:** Jifunze zaidi kuhusu mtandao wa vituo vya Telegram vilivyokuwa vikishiriki ujumbe wa kutisha dhidi ya mwandishi wa habari wa ndani nchini Ujerumani.




Bonyeza hapa kusoma taarifa yote.

# 4 Weka bayana kile kinachosemwa

**Kutambua hoja zinazosambazwa na shambulio la upotoshaji kunaweza kusaidia kufichua lengo lililokusudiwa na kampeni.**

### Fanya uhakiki wa ukweli juu ya kinachodaiwa na mashambulizi

- Tambua na fanya uhakiki juu ya habari za uwongo zilizotumika katika shambulio kuhusu kituo cha habari na uhusiano wake wa kisiasa, ufadhili au taarifa nyingine za shirika.
- Kuwa makini kwamba kampeni za upotoshaji wakati mwingine zinahusisha kazi za awali za waandishi wa habari ambazo hazihusiani moja kwa moja na kazi ya uandishi wa habari iliyotumika kuchochea kampeni ya uchafuzi wa jina.

### Utambuaji wa hoja za Habari potofu


- Fanya uchambuzi wa maudhui ya machapisho ya mitandao ya kijamii na makala za vyombo vya habari na hotuba za umma
- Angalia maneno na misemo iliyotumika, zingatia maneno na misemo mipya iliyotumika.
- Tumia hazina ya habari za upotoshaji iliyopo katika ukurasa wa European Digital Media Observatory (EDMO) (Ulaya) na unganisha matokeo yako na habari zilizopo za upotoshaji.

**VITU VYA KUFANYA**

## Tengeneza mitandao ya habari za upotoshaji na fuatilia habari hizo kwa muda. Aina hii ya uchambuzi inatoa muhtasari wa jinsi habari hizo dhidi ya waandishi wa habari zinavyohusiana na kusambazwa katika vituo vile vile na wakati mmoja, na kukupa uelewa kamili wa habari hizo kwa upana zaidi

Nyenzo nyingi zinazoweza kutengenza mitandao wa habari potofu hutegemea Akili Mnemba. Katika hili tafadhali hakikisha unafuata misingi ya uwazi juu ya matumizi ya teknolojia ya Akili Mnemba katika vyumba vya habari. Kuna miongozo kadhaa lakini unaweza kuanza na kanuni za Ushirika katika Akili Mnemba ambazo unaweza kuzipata hapa.

**Mfano:** Jifunze zaidi kuhusu mitandao ya habari na nadharia potofu zinazotangazwa na kusambazwa kupitia Telegram nchini Uhispania.




[Bonyeza hapa kusona ripoti kamili.]

**VITU VYA KUFANYA**

## Tengeneza ripoti juu ya uchunguzi huu. Kwa kufuata miongozo hii utaweza kutambua vipengele vikuu vinavyounda kampeni ya upotoshaji na kutoa jibu kwa maswali makuu ya kiuandishi wa habari: Nini? Nani? Kwa nini? Jinsi gani? Lini? Wapi?

Sambaza ripoti kwa wadau muhimu kitaifa na kimataifa kama vile vyama vya waandishi wa habari.

Kabla ya kufanya hivyo zingatia hatari zozote za kisheria (k.m. ongea na vyama vya waandishi wa habari kwa ushauri wa kisheria au na idara ya kisheria ya kituo chako cha habari). Kwa kuwa ripoti zinaweza kuleta majina ya wale waliotambuliwa kuwa nyuma ya mashambulizi, kuna uwezekano wa watu binafsi au makampuni kushtaki kwa kashfa?

# Vyanzo Vingine vya Msaada

## Amnesty International: Citizen Evidence Lab

“Mtandao huu unalenga kusaidia mashirika ya haki za binadamu, watafiti, wachunguzi, wanafunzi, waandishi wa habari na wengine kuchunguza na kuwapatia mbinu za uchunguzi wa kidijitali kwa ajili ya utafiti wa haki za binadamu.”

Tembelea ukurasa hapa.

## Zana za Uchunguzi wa Kimtandao za Bellingcat

“Zana hii ya mtandaoni ya uchunguzi wa wazi inajumuisha mwongozo juu ya huduma za satelaiti na ramani, zana za kuthibitisha picha na video, tovuti za kuhifadhi kurasa za wavuti na mengi zaidi.”

Tembelea vitu vyao hapa.

## Maabara ya Utafiti wa Forensiki wa Kidijitali

“Programu inajumuisha warsha na vipindi vya mafunzo vya vitendo vinavyoshughulikia elimu ya vyombo vya habari, mbinu za uchunguzi wa wazi, uthibitishaji wa chanzo, uchambuzi wa habari zinazosambazwa, ufuatiliaji wa mitandao ya kijamii, utambuzi wa eneo na mada nyingi nyingine.”

Tembelea rasimali zao hapa.

## European Digital Media Observatory (EDMO): Mafunzo

“EDMO inatoa mada za mafunzo ya mtandaoni mara kwa mara zinazolenga kusaidia wadau tofauti kuelewa na kushughulikia upotoshaji wa mtandaoni.”

Tembelea program yao ya mafunzo hapa.

## Tactical Tech: Exposing the Invisible

“Exposing the Invisible inaangalia mbinu, zana na njia tofauti pamoja na mazoea ya mtu binafsi ya wale wanaofanya kazi katika mawamba mapya ya uchunguzi.”

Tembelea ukurasa wao hapa.

## Verification Handbook for Disinformation and Media Manipulation, na Craig Silverman

“Kitabu hiki kinawawezesha waandishi wa habari na maarifa ya kuchunguza akaunti za mitandao ya kijamii, bots, programu za ujumbe binafsi, operesheni za taarifa, video bandia pamoja na aina nyingine za upotoshaji na udanganyifu wa vyombo vya habari.”

Pakua jarida hapa.

**Mradi**

# Kuchanganua mbinu za habari potofu zaki-populism Ulaya

**IPI Taz na Faktograf wanafanya kazi pamoja kuchanganua propaganda ya populism huko Ulaya inayolenga wahakiki ukweli na waandishi wa habari za kichunguzi - ambao ni wadau muhimu katika vita dhidi ya upotoshaji.**

European MEDIA AND INFORMATION Fund
Managed by
Calouste Gulbenkian Foundation

*Mradi wa* ***Kuchanganua mbinu za habari potofu zaki-populism Ulaya*** *unaungwa mkono na European Media and Information Fund, na kusimamiwa na Calouste Gulbenkian Foundation.*

*Mwongozo umetayarishwa na Tajana Broz (Faktograf) na Javier Luque Martínez (IPI).*

*Angalizo:*
*Uwajibikaji wa maudhui yoyote yanayoungwa mkono na European Media and Information Fund upo kwa waandishi wenyewe na si lazima ushabihiane na msimamo wa EMIF na Washirika Wahisani wa Mradi, Calouste Gulbenkian Foundation na European University Institute.*

In partnership with Canada

*The translation of this resource was coordinated by the IPI Africa program, with the support of the Government of Canada's Office of Human Rights, Freedoms and Inclusion (OHRFI).*